# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI TANGU KUANZISHWA KWA RUWASA HADI SASA NA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2022/23

## 1. Utangulizi

RUWASA ilirithi jumla ya **skimu 1,379** zilizokuwa zimekamilishwa na Halmashauri za Wilaya mbalimbali zilizokuwa chini ya usimamizi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kati ya skimu hizo, **skimu 177** zilikuwa na changamoto za utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi na **skimu 1,202** zilikuwa zimekamilka na zinaendelea kusimamiwa na RUWASA chini ya Wataalamu waliopo kwenye vyombo vya Watumia Maji vilivyosajiwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

Vilevile, RUWASA ilirithi jumla ya **miradi 632** iliyokuwa inaendelea na utekelezaji ambapo kati ya miradi hiyo, **miradi 566** imekamilishwa chini ya usimamizi wa RUWASA na **miradi 66** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Hata hivyo, baada ya kuanzishwa kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kumesaidia uibuaji wa **miradi mipya 912** ambapo kati ya miradi hiyo, **miradi 403** imekamilishwa na imeshaanza kutoa huduma ya maji watu **wapatao 1,851,300** na **miradi 503** ipo katika hatua mablimbali za utekelezaji

## 2. Utekelezaji Wa Miradi ya Maji Katika Kipindi Cha Mwaka Wa Fedha 2021/22

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilipanga kutekeleza jumla ya miradi **1,527** ya maji na Usafi wa mazingira ambapo serikali ilitenga **Shilingi 422,928,757,364.00** kwa ajili ya utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, miradi **1,176** inahusisha ukamilishaji wa miradi iliyokuwa inaendelea, miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji. Miradi **351** inahusisha utafutaji wa vyanzo vya maji na maandalizi ya miradi mipya kwa ajili ya utekelezaji wa mwaka wa fedha 2022/23. Vilevile, Serikali ilipanga kukarabati na kujenga mabwawa **19**.

Sambamba na hilo, katika kuhakikisha kuwa huduma ya maji katika mikoa inaimarika, Serikali ilitoa bajeti ya nyongeza ya **Shilingi 78,528,753,850.00** kupitia Mpango wa Mapambano Dhidi ya UVIKO– 19 kwa ajili ya kutekeleza **miradi 172** ya maji vijijini. Utekelezaji wa miradi katika mikoa yote nchini upo katika hatua mbalimbali na matarajio yetu ni kuikamilisha ifikapo mwishoni wa mwezi Juni, 2022.

Aidha, hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Serikali kupitia Wakala wa maji na usafi wa Mazingira (RUWASA) imefanikiwa na inaendelea kufanya yafuatayo: -

i. Kukamilisha ujenzi wa miradi ya maji **303** ambapo wananchi wapatao **1,467,107** wanapata huduma ya maji kupitia vituo vya kuchotea maji **4,147** vilivyojengwa katika vijiji mbalimbali.

ii. Kuendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi **873** ambapo kati ya miradi hiyo, **225** inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022 na miradi **648** itaendelea na utekeleza katika mwaka wa fedha **2022/23.**

iii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi **172** ya Uviko -19 inayotarajiwa kugharamu **Shilingi 78,803,215,410** na inatarjia kukamilika ifikapo Juni, 2022. Kukamilika kwa miradi hiyo, kutanufaisha wananchi wapatao **1,036,071** waishio katika vijiji **307.**

iv. Kuendelea kukwamua **miradi 42** yenye changamoto ya maji na kurejesha huduma ya maji kwa wananchi wapatao **186,512**. Aidha, kukamilishwa kwa miradi hiyo kumewezesha idadi ya miradi iliyopatiwa ufumbuzi kuongezeka kufikia miradi **127** kati ya miradi **177** iliyoripotiwa awali ambayo ni **asilimia 71.8** ya miradi yote yenye changamoto. Sambamba na hilo, kwa miradi iliyobaki RUWASA imepanga kuikamilisha kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

v. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kwa kutumia utaratibu wa *force account* baada ya kubaini kuwa kasi ya Wakandarasi imeanza kupungua. Hadi sasa, zaidi ya **miradi 439** imeshakamilisha wa kutumia utaratibu huo ambapo zaidi ya **Shilingi bilioni 265** zimetumika kwa ajili ya miradi hiyo.

   Kwa **miradi 86** iliyotangaziwa Makao Makuu ya RUWASA ilikuwa itekelezwe kwa gharama ya **Shilingi 367,310,874,913.66,** lakini baada ya majadiliano na makubaliano na Wakandarasi gharama hizo zilipungua hadi kufikia **Shilingi 309,905,697,188.44**. Hivyo, Serikali imefanikiwa kuokoa jumla ya **Shilingi 57,405,177,725.22** sawa ya **asilimia 15.6** ya fedha iliyokusudiwa kutumika kabla ya makubaliano.

**Mapokezi na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/22**

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imepokea jumla ya **Shilingi 390,857,233,773** na hadi kufikia Mwezi Machi, 2022 utekelezaji wa miradi umetumia jumla ya **Shilingi 161,484,018,119** sawa na **asilimia 41.3**.

## 3. Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji

kufuatia jitihada zilizofanywa Wizara ya Maji kupitia RUWASA hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 kimesaidia kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kufikia **asilimia 74.5** ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 64.8** mwaka 2019 tangu RUWASA ilipoanzishwa ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 9.7** kwa kipindi cha miaka miwili. Kasi hii, ni nzuri na tukienda kwa kasi hii, tunatarajia kufikia **asilimia 85** ifikapo mwaka 2025, kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

## 4. Mpango wa Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka Wa Fedha 2022/23

Katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imepanga kutekeleza jumla ya miradi ya maji **1,029** ambapo miradi **648** ni miradi inayoendelea kutekelezwa na miradi **381** ni miradi mipya. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya utekeleza miradi hiyo ni **Shilingi 387,736,591,242.**